Ushirika katika Njia ya kuelekea kwenye Ufalme.

TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUTAFUTA KUMBUKUMBU REJEA ZOTE.

Shabaha ya ajabu ya Mungu kwa wanaume na wanawake wa nyakati zote ni Ufalme wa Mungu katika dunia hii. Wakati wa maajabu na shughuli kubwa kama tutakavyoona katika somo la mada hii. Lile utakalofanya wakati huu kuwa ni la kipekee ni umbile la wale wote wanaofuata sheria ya Mungu kwa uaminifu ambapo hivi sasa tunayakuta katika mafundisho ya Yesu. Umbile letu hivi sasa ni halisi ikiwa na maana kuwa tunazeeka na kufa. Ahadi ya Mungu kupitia kwa Yesu ni kuwa katika Ufalme wake hatutakufa lakini tutakuwa na umbile la kiroho. Paulo Mtume wa Yesu alieleza haya katika Waraka wa kwanza kwa Wakorintho kifungu cha 15. Soma kutoka mstari wa 35 hadi mwisho wa kifungu hiki na utabaini kuwa Paulo alitumia mfano huu wa mbegu iliyopandwa katika udongo. Katika wakati muafaka mbegu inachipusha majani ya kijani juu ya uso wa ardhi na maisha mapya ya mmea huanza.

Halikadhalika tumepewa ahadi hii ya ufufuko iliyotolewa kwetu na Mungu ikiwa ni malipo ya imani na utiifu wetu. Utakuta mfano ambao Paulo anatupa katika mistari ya 51 na 58 kuwa ni ya kututanabaisha. Iwapo utakuwa bado haujaamua kubatizwa, hili litakuwa ni jambo litakalo kusaidia kuamua.

Mara nyingi katika Biblia tunakuta waandishi wakielezea maisha kama safari, na hii ni njia nzuri ya kutafakari juu ya hili. Angalia katika Injili ya Mathayo sura ya 7 mistari ya 13 na 14. Katika mfano huu Yesu alielezea safari ya kuelekea Ufalme wa Mungu kama njia nyembamba ambapo dunia nzima wanakimbilia kwenye njia pana ambayo ni nyepesi inayoongoza kwenye kifo cha milele,sisi kama wafuasi wa Yesu kwa uangalifu tunafuata njia nyembamba tukiwa tunajaribu kuvuka vikwazo tukijaribu kutokuondoka katika njia nyembamba ili tusipotee. Kama unaangalia sasa katika Injili ya Yohana sura ya 14 mstari wa 6 utakuta kwamba Yesu anajisemea kuwa yeye ni njia hivyo ushauri anaoutoa ni mzuri. Kama tutamtumaini katika maisha yetu, kufuata mfano wake na sheria zake, njia nyembamba itakuwa rahisi na muhimu kutuwezesha kupita kwa usalama.

Kwa watu wengine kutembea katika njia hii kuelekea kwenye Ufalme sharti kufanyike bila ya kuwashirikisha binadamu. Hakuna mitume wengine waishio
Umbali wa kusafiri au kuishi katika nchi iliyoathirika na vita ambapo itakulazimu kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kuepuka matatizo.

Kwa sisi tunaoishi katika sehemu zenye amani zaidi katika dunia hii, inawezekana kubatizwa na kuungana na ndugu katika Kristo (wakristadelfia) katika liletunaloita Ecclesia. Hii ina maana ya kwamba, kwa kutumia mfano wa Yesu, tunaweza kusafiri hadi kwenye Ufalme wa Mungu tukiungana na watu wengine wenye imani kama sisi.

Unaposoma neno "Kanisa" katika Agano Jipya, neno la asili la Kigiriki lililotumiwa na Yesu na Mitume wakati wote ilikuwa "Ecclesia" na Wakristadelfia wamechagua kutumia neno lile la Kigiriki kama kikundi chao cha ndugu wanaume na Wanawake.

Wakati Mwanafunzi wa Yesu aliyebatizwa hana uchaguzi bali kuwa pekeyake, ni muhimu kumtegemea Mungu halikadhalika na Yesu kupitia Sala za kila siku na kusoma Biblia. Hali hii ikijitokeza, ndugu sharti aulize maswali, "Kwa nini niko pekee yangu? Je ni kwa sababu sitaki kuwa pamoja na wengine? Kwa nguvu kidogo au kwenda katika mji tofauti je inawezekana kuungana na Wakristadelfia wengine katika kuumega mkate?.

Katika hali nyingine, jambo hili bado halitawezekana na kwa bahati nzuri kuna njia nyingine. Daima ni jukumu la Mwanafunzi kuhusika katika uelewa/ufahamu ambao ni nyeti atakapokuwa amepata na kuwaambia wengine juu ya jambo hilo. Waambie wengine juu ya imani na matumaini yako makubwa katika Yesu. Kwa njia hii unaweza kukusanya kikundi kipya cha waumini katika mji wako au kijiji.

Yesu alitarajia Wanafunzi wake kukusanyika pamoja katika vikundi ili waweze kuabudu pamoja. Wangeweza kumkumbuka Yesu pamoja katika Mkate na Divai na kusaidiana katika njia hii kuelekea katika Ufalme. Sio vizuri kusafiri pekee yako, mara kwa mara ni rahisi na ni salama kuwa na wenzako.

Mwanzoni mwa huduma yake Yesu hakutembea pekee yake, aliwachagua Mitume kumi na wawili na siku hadi siku alitembea na wanaume na wanawake wengi. Paulo aliposafiri katika nchi nyingi kuhubiri Injili, hakuwaacha nyuma ndugu, wanaume kwa wanawake wakiwa wamejitenga, aghalabu alianzisha Makanisa mapya mahali ambapo wanafunzi wangeweza kusaidiana. Angalia

katika waraka wa pili wa Paulo kwa Wathesalonike sura ya 1 mistari ya 3 hadi 5. Hususani katika nyakati ngumu, ni nzuri kusaidia kubeba mizigo ya wengine.

Inakupasa kuelewa kwamba kama umebatizwa utakuwa kaka au dada katika Kristo na sehemu ya kukaribishwa kwako kuwa kiungo cha Ecclesia iliyokaribu nawe na mjumbe wa familia kubwa ya Wakristadelfia duniani. Kama kuna ecclesia nyingi karibu na wewe, unaweza kuchagua uwe wapi.

Ecclesia zote zinajiendesha zenyewe na kuna kikundi cha wazee ambao ni ndugu wenye uzoefu watakao kuwa na madaraka ya kuendesha shughuli za kila siku. Aidha, wakati muda muafaka, ecclesia nzima itakutana kujadili juu ya mambo mazito zaidi yanayokihusu kikundi na mara moja kwa mwaka ili kuchagua wazee watakao hudumu katika mwaka ujao.

Uchaguzi katika makundi makubwa unaweza kuwa kwa kura ya siri. Pia Katibu na Mweka Hazina huchaguliwa. Wakati mwingine Katibu huitwa ndugu mwandishi kwa sababu ni wajibu wake wa kuweka kumbukumbu zote za mikutano.

Kwa njia hii ecclesia ina demokrasia kamili na waumini wote wanahusika katika maamuzi. Wote wako sawa mbele ya Mungu na hakuna wachungaji, Mapasta au wainjilisti miongoni mwetu. Elimu yetu ya Biblia inapatikana kutokana na kila mmoja wetu kujisomea. Kuhusu ndugu, kuna haja ya kuandaa uimarishaji na mafunzo maalumu ya madarasa ya Biblia na Makundi ya kujifunza. Halikadhalika, wanawake pia wanatakiwa kuandaa masomo ikiwa wanafundisha katika madarasa ya Jumapili (Sunday school) au madarasa ya wanawake. Hakuna anayevaa nguo maalumu, hakuna majoho au kola ya shingoni kwa ndugu na vyeo maalumu mbali ya vile vilivyoelezwa. Wote wanafanya kazi pamoja katika njia rahisi mbele ya Mungu. Jumuiya ya Wakristadelfia ambayo hivi sasa inazungukwa na ndugu yaani wanaume na wanawake katika nchi nyingi wanaungana katika imani yao kwa maelezo ya kawaida ya imani.

Ecclesia nyingine zimejengeka katika misingi ya maoni ya mila nzito na hizi husawazishwa na nyingine ambazo zina maoni ya kisasa zaidi. Nyingi za ecclesia zina maoni nusu kati ya tofauti hizi na mafunzo yote ya Biblia kati yetu ni suala la majadiliano ya mara kwa mara. Hii inasaidia udugu duniani pote kuwa na imani ya aina moja na kuabudu ambako kungeeleweka kama nguvu kubwa moja.

Kama Mkristadelfia aliyebatizwa, unaweza baadaye kusafiri katika sehemu nyingine za dunia ambako unaweza kuabudu na ndugu zako katika njia utakazo kuwa umezizoea kabisa.

Taarifa hii kuhusu muundo wa ecclesia za Wakristadelfia imejumuishwa katika somo hili kwa sababu ni muhimu kwamba unaelewa thamani kubwa ya kuwa katika ecclesia wewe mwenyewe kuweza kumwabudu Mungu pamoja na wengine walio na imani kama yako. Unaweza kuongeza nguvu zako katika kuunganisha kazi ya uhubiri na kuwahudumia wengine ambayo ni sehemu muhimu ya maagizo ya Yesu kwetu sisi.

Mara nyingi ni kweli kwamba ndugu anapokuwa hayupo katika ecclessia kwa majuma kadhaa, na hivyo kutokujiunga katika huduma ya chakula cha Bwana (Mkate na Divai) katika kumkumbuka Yesu. Imani yao binafsi inaweza kuanza kuteteleka.

Inakuwa vigumu kwao kuishi katika njia ile nyembamba iendayo katika Ufalme. Imani ni mwaka wa moto unayohitaji kulishwa chakula cha kiroho mara kwa mara. Matunzo na kulishwa tayari vinapatikana katika ecclesia; ni vigumu sana kuvipata ukiwa pekee yako.

CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)